## Maswali

1. Mbona ndugu wa Yusufu walienda Misri?
2. Ndugu yupi alibaki nyumbani na Yakobo?
3. Ndugu waliinamia nani huko Misri?
4. Mbona Yusufu alizungumza na nduguze kwa ukali?
5. Yusufu alisema nduguze walikuwa wamekuja nini Misri?
6. Yusufu alizuilia ndugu yupi gerezani?
7. Yusufu alitaka nduguze wakuje Misri tena na nani?
8. Ndugu walipata nini kwa mifuko yao walipofika nyumbani?
9. Mbona ndugu walirudi Misri?
10. Nini ilifanyika walipokuwa wakila chakula na Yusufu?

## Majibu

1. Walienda Misri kununua chakula kwa sababu ya njaa.
2. Benyamini, mwana mdogo alibaki nyumbani na Yakobo.
3. Ndugu waliinamia mtawala –na huyo alikuwa Yusufu.
4. Yusufu alitaka kujua kama nduguze walikuwa wamebadilika.
5. Yusufu alisema kwamba nduguze walikuwa wamekuja kupeleleza nchi ya Misri.
6. Yusufu alizuilia Simeoni gerezani.
7. Ndugu walikuwa waje na Benyamini ikiwa watarudi Misri tena.
8. Ndugu walipata pesa zote ndani ya mifuko zao.
9. Ndugu walirudi Misri kwa sababu hawakukuwa na chakula cha kukula.
10. Ndugu walikalishwa kulingana na umri wao. Benyamini alipewa chakula mara tano zaidi ya ndugu wengine.

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

## Awamu ya 2    Mwaka wa 1

# 14 Nduguze Yusufu wanakuja Misri

**Kwa Biblia** Mwanzo 42 na 43

### Somo

Kuonyesha kwamba Mungu alilinda Yakobo na familia yake wakati wote wa njaa. Mungu alitimiza kuzudi lake kwa watu wake.

### Kiini cha somo

Kwa miaka saba, Misri ilikuwa na mavuno mazuri. Yusufu aliweka nafaka nyingi isiyoweza kuhesabika. Baadaye kukawa na njaa nyingi kwa miaka saba. Hakuna kilichomea chochote.

Kando na Misri, nchi zingine zilikuwa na njaa pia . Nchi ya Kanaani ilikuwa na njaa kubwa. Yakobo na wanawe kumi na moja hawakukuwa na chakula.

Yakobo alisikia kwamba kuna chakula kingi katika Misri. Alituma wanawe kumi wakubwa Misri ili wanunue chakula. Yakobo alibaki na mwanawe mdogo Benyamini nyumbani. Benyamini alikuwa mwana wa Raheli mkewe mpendwa.

Kwa siku nyingi ndugu kumi walisafiri kwenda katika nchi ya Misri. Walipelekwa kwa mtawala wa Misri na wakamwinamia. Mtawala wa Misri alikuwa Yusufu!

Ndugu hawakumtambua Yusufu. Miaka mingi ilikuwa imepita tangu wamuone. Yusufu alikuwa na miaka kumi walipomuuza Misri na sasa alikuwa mtu mzima. Yusufu alivaa na kuzungumza kama Mmisri. Ndugu zake walijua Yusufu kama mtumwa na hawezi kuwa Mtawala wa Misri. Nduguze walikutana na Yusufu lakini hawakumtambua.

Yusufu aliwatambua ndugu zake papo hapo. Lakini alijifanya kwamba hawajui. Hakuwambia kwamba yeye ni Yusufu. Yusufu alitaka kujua kama wamebadilika baada ya hizo miaka mingi. Alitaka kujua kama wangali katili au wamekuwa wazuri. Tena Yusufu alikuwa anatafuta njia ya kumleta babake Yakobo na nduguye mdogo Benyamini hadi Misri.

Yusufu hakuzungumzia ndugu zake vizuri. Aliwambia, “Nyinyi ni wapelelezi. Mmekuja kupeleleza nchi ya Misri.” Nduguze walimwambia kwamba wao si wapelelezi. Walikuwa wamekuja Misri kununua chakula kwa sababu ya njaa. Walimwambia. “Sisi ni ndugu kumi. Tulikuwa ndugu kumi na mbili, mdogo ako nyumbani na baba yetu. Ndugu mwingine alikufa.” (Ndugu hawakutambua kwamba mtu waliokuwa wakizungumza naye ndiye ndugu yao waliofikiria alikufa!)

Yusufu alijifanya kwamba hakuamini nduguze. Aliwaweka wote gerezani kwa siku tatu. Mara tena walipelekwa kuona Yusufu. Aliwambia, “Nataka nijue kama mko mnaniambia ukweli. Nitamzuia mmoja wenu gerezani hapa. Wengine wenu mnaweza kupelekea familia zenu chakula nyumbani. Mkirudi Misri kuchukua chakula tena, lazima mkuje na ndugu wenu mdogo. Nitakapoona ndugu wenu mdogo, nitajua mnaniambia ukweli. Msirudi kwa nchi ya Misri tena msipokuwa na ndugu wenu mdogo.”

Simeoni alibaki Misri gerezani. Ndugu wengine tisa walichukua mifuko zao za chakula na kwenda nyumbani. Waliambia Yakobo yote yaliyotendeka. Yakobo alihuzunika sana. Alikataa kumwajilia Benyamini aende Misri. Ndugu walifungua mifuko waliyobebea chakula kutoka Misri. Pesa walizoenda nazo Misri kununua chakula zilikuwa ziko ndani ya mifuko. Mtu alikuwa amerudisha pesa zote ndani ya mifuko yao. Waliogopa sana.

Yakobo hangeajilia Benyamini aende Misri na nduguze. Ndugu walikaa na familia zao Kanaani. Simeoni alikaa gerezani Misri.

Baada ya mda chakula chote kilikwisha. Njaa nyingi ilikuwa bado Kanaani kwa nchi aliyokaa Yakobo na familia yake. Baada ya muda kila mtu alikuwa na njaa. Ndugu waliendelea kuhimiza Yakobo kwamba waende Misri chakula. Walitakiwa wanunue chakula. Mwishowe Yakobo alikubali.

Lakini hawangeenda Misri bila kuchukua Benyamini. Yakobo alifadhaika na kuhuzunika. Alisema kwamba atakufa ikiwa kitu chochote kitafanyika kwa Benyamini huko Misri. Yakobo aliomba Mungu awalinde na awarudishe salama nyumbani.



*Picha hii ilipatikana Misri ndani ya kaburi mzee*
*Watu wageni kama nduguze Yusufu wanazuru Misri.*

Ndugu kumi na moja walisafiri kwenda nchi ya Misri. Walibeba zawadi kumpelekea mtawala wa Misri. Walichukua hata na pesa zilizopatikana kwa mifuko yao walipoenda mara ya kwanza. Walienda na pesa zingine nyingi kununua chakula. Walipofika Misri, walipelekwa kwa nyumba ya mtawala. Waliambiwa kwamba watakula chakula pamoja na mtawala.

Yusufu alizungumza na nduguze akitumia mkalimani. Nduguze hawakujua lugha ya kimisri. Bado Yusufu hakutaka nduguze wamjue. Kwa hivyo alijifanya kwamba hasikii lugha ya kiebrania.

Yusufu aliuliza nduguze hali ya baba yao. Walikaa chini wakala chakula. Yusufu aliketisha nduguze mezani kufuatana na umri wao. Walishangaa - mtawala alijuaje umri wao? Chakula kilipoletwa, Benyamini alipata mara tano zaidi ya ndugu wengine. Hawakuelewa kilichokuwa kikiendelea.

Tutamaliza hadithi hii kwa somo lijalo.